| 6 | **AUTOMOTIVE ENGINEERING DEPARTMENT**<br>i).Diploma in Automotive Engineering Module I<br>ii). Diploma in Automotive Engineering Module II<br>i) Craft in Automotive Engineering Module II | 1 Year | KCSE Mean Grade D+<br><br>Pass in Dip. Mod. I<br><br>Pass in craft I | | | KNEC |
| 7 | **ELECTRICAL/ELECTRONICS ENGINEERING DEPARTMENT**<br>i) Diploma in Electrical and Electronics Engineering (Power & Telecommunication Option) Module III<br>ii) Diploma in Electrical and Electronics Engineering (Power & Telecommunication) Module II<br>iii) Diploma in Electrical and Electronics Engineering (Power & Telecommunication) Module I<br>iv)Craft Certificate in Electrical and Electronics Engineering Module I | 1 Year | Pass in Dip. Mod. II<br><br>Pass in Dip .Mod. I<br><br>KCSE Mean Grade C-<br><br>KCSE Mean Grade D | | | KNEC |
| 8 | **FOOD AND BEVERAGE DEPARTMENT**<br>I).Diploma in Food and Beverage Management Module II<br>ii). Craft in Food and Beverage Sales and services Module I | 1 Year | Pass in Module I<br>KCSE Mean Grade D<br>KCSE Mean Grade D | | | KNEC |

**INDUSTRIAL SKILLS UP-GRADING COURSES**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | **BUILDING & CONSTRUCTION DEPARTMENT**<br>i) Plumbing Basic | 3 months | School leavers, employees from SMEs & SMIs, Employees from Industries | 1st Term 32,500/= Subsequent terms 25,500/= | 1st Term 23,000/= Subsequent terms 16,000/= | NITA KITI |
| 11 | **CLOTHING & TEXTILES DEPARTMENT**<br>i). Dress Making Basic (Including tie & dye and Embroidery)<br>ii). Tailoring Basic (Including tie & dye Embroidery)<br>iii). Hair Dressing & Beauty Therapy | | | | | NITA KITI |
| 12 | **MECHANICAL ENGINEERING DEPARTMENT**<br>i)Welding & Fabrication<br>ii) Lathe Machine Operator<br>iii) General Fitting | | | | | NITA KITI |
| 13 | **AUTOMOTIVE ENGINEERING DEPARTMENT**<br>i). Motor vehicle mechanics (Advance | | Pass in MVM (intermediate) | | | NITA KITI |
| 14 | **FOOD & BEVERAGE DEPARTMENT**<br>i) Certificate in Food & Beverage<br>ii) Production, Sales & Service | 3 months | School leavers, Employees from Industries | | | KITI |
| | **TAILOR MADE COURSES**<br>ii) Juice Making<br>iii) Yogurt Making<br>iv) Jam Making | 3 Days | | 6,000/= | 6,000/= | KITI |
| 15 | **ELECTRICAL/ ELECTRONICS ENGINEERING DEPARTMENT**<br>i). Electrical Installation basic intermediates and Advance,) | 3 months each | School leavers and employees from industries | 1st Term 32,500/= Subsequent terms 25,500/= | 1st Term 23,000/= Subsequent terms 16,000/= | KITI NITA |
| | ii) Solar Water Heating<br>iii) Solar PV Technology | 3 months Evening and weekends | Pass in Electrical Installation course, Practicing solar marketers or Electrical | | | KITI NITA |
| 16 | **I.C.T. DEPARTMENT**<br><br>Computer Proficiency Course | 3 months | School leavers and employees | 1st Term 32,500/= Subsequent terms 25,500/= | 1st Term 23,000/= Subsequent terms 16,000/= | KITI |
| | **Computer Aided Design**<br>i) AutoCAD<br>ii) Autodesk Inventor<br>iii) Civil 3D | 1 month each | Builders, Draughtsmen, Engineers, Technicians working in manufacturing industries | 50,000/= | 50,000/= | |
| 17 | **LEATHER & TANNERY DEPARTMENT**<br>i). Leather Tanning (Basic)<br>ii). Footwear ( shoe making) Production (Basic)<br>i). Leather work (Basic) | 3 months each | Employees from tanneries, shoe industries, school leavers | 1st Term 32,500/= Subsequent terms 25,500/= | 1st Term 23,000/= Subsequent terms 16,000/= | KITI NITA |

All applications MUST be accompanied with Photocopies of:-

- KCSE Certificate or Result Slip
- School Leaving Certificate or any relevant certificates
- National ID Card
- Birth Certificate
- Money Order/ Postal Order of Kshs. 300 (Non-refundable) application fee
- 1 passport size photograph (colored)

**APPLICATIONS SHOULD BE ADDRESSED TO:**
**THE DIRECTOR**
**KENYA INDUSTRIAL TRAINING INSTITUTE**
**P.O. Box 280-20100 Nakuru, Tel. (051)2216755,**
**E-mail: directorkiti@yahoo.com Mobile numbers: 0774944615**
**TO REACH US ON OR BEFORE 30TH AUGUST 2023**

KENYA VISION 2030

# JKUAT, Wachina kuimarisha utoshelevu wa chakula kupitia uzalishaji wa mtama

NA PATRICK AMUNAVI

Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta (JKUAT) na washirika wao kutoka Chuo cha Sayansi cha China wanawahimiza wakulima wa Kenya kukumbatia teknolojia ya kilimo yenye ufanisi ya mtama wa aina ya Foxtail kutoka China ili kukabiliana na ukosefu wa chakula nchini.

Mtama aina ya Foxtail kutoka China ni matunda ya utafiti wa ushirikiano kati ya watafiti kutoka JKUAT na washirika wao kutoka China. Prof. David Mburu anaongoza watafiti wa JKUAT kutoka Chuo cha Kilimo na Maliasili (COANRE) huku Prof. Xiaoxin Li na Suyin Chen wakitoka katika Kituo cha Utafiti wa Maliasili za Kilimo (CARR), Taasisi ya Jenetiki na Maendeleo ya Biolojia (IGDB), Chuo cha Sayansi cha China (CAS).



Wakulima katika shamba kielelezo katika JKUAT wakijifunza namna ya kuzalisha mtama kutoka Uchina aina ya Foxtail.

Akizungumza na wakulima kutoka Kaunti ya Kiambu, Prof. Mburu alipongeza juhudi za ushirikiano na CAS kupitia Kituo cha Utafiti wa Maliasili za Kilimo

> China ni nchi yenye watu wengi lakini inazalisha chakula kinachotosha wote-Mburu

kuhusu "utafiti na mafunzo ya wanafunzi wa shahada ya uzamili."

Akirejelea mtama aina ya Foxtail kutoka China, Prof. Mburu aliwaeleza wakulima kuwa kuna mengi ya kujifunza kutoka China, nchi ambayo ina idadi kubwa ya watu lakini inazalisha chakula cha kutosha.

Aliwahimiza pia wakulima kuzingatia kilimo cha mtama wa aina ya Foxtail ili kushughulikia utoshelevu wa chakula nchini. Prof. Xiaoxin Li alisema mafunzo hayo yalikuwa fursa "ya kushirikiana maarifa na wakulima wa Kenya kuhusu teknolojia ya kilimo na usimamizi wenye ufanisi wa mtama wa aina ya Foxtail kutoka China ambao ni maarufu sana nchini China."

Prof. Li aliwaambia wakulima kuwa mtama unakuzwa zaidi kaskazini mwa China, akitaja faida za mazao hayo ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuhimili ukame, uwezo wa kuhifadhi maji (ukilinganisha na mazao kama mahindi na mpunga), ufanisi mkubwa wa matumizi ya virutubishi, na uwezo wa kuhimili magonjwa.

Pia, alisema mtama aina ya Foxtail hukua vizuri kwenye udongo aina ya 'loam na sandy loam' na akaongeza kwamba mmea huo "unakua haraka zaidi kwa joto kati ya digrii 24-25 Celsius." Prof. Li alitaja mtama huo kama "mmea unaokuwa katika muda mfupi unaohitaji mwangaza mdogo wa jua.

Aliorodhesha bidhaa za chakula zinazotokana na mtama huo kama vile sushi ya Kijapani, uji, vitafunio, divai ya mtama na bidhaa nyingine ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa chakula cha wanyama.

Watafiti walifichua kuwa "kilimo cha mtama aina ya Foxtail kinawezekana zaidi katika sehemu nyingi za Kenya ya Kati na Mashariki, ikiwa ni pamoja na Kaunti za Nyeri, Machakos, Makueni, na Kiambu."

---

REPUBLIC OF KENYA

## COMMODITIES FUND

COMMODITIES FUND
Financing Crops for Prosperity

### NAFASI ZA KAZI

Commodities Fund (ComFund) ni shirika la Serikali lililoanzishwa chini ya Sheria ya Mimea, 2013 chini ya Wizara ya Kilimo na Ustawi wa Mifugo, kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa sekta ya mimea nchini. ComFund ingependa kusajili watu wenye uzoefu, wa kujituma na wachapakazi, kujaza nafasi zifuatazo:

| S/N | CHEO | NO. |
|---|---|---|
| 1. | ICT Manager | Nafasi 1 |
| 2. | Internal Auditor | Nafasi 1 |
| 3. | Executive Secretary / Personal Assistant to the Managing Trustee/ CEO | Nafasi 1 |
| 4. | Credit Officer | Nafasi 3 |
| 5. | System Auditor | Nafasi 1 |
| 6. | Credit Assistant | Nafasi 1 |
| 7. | Audit Assistant | Nafasi 1 |

Maelezo ya kina kuhusu nafasi ya kazi yamo kwenye wavuti wa ComFund's website; www.comfund.co.ke

**NJIA YA KUTUMA MAOMBI**

Wale wanaotimiza matakwa ya kazi hizo wanapasa kutuma maombi yao ya kazi: CV pamoja na stakabadhi zingine za masomo, vyeti vya kitaaluma pamoja na anwani za marefarii wao kwa:

**Managing Trustee/CEO,**
**Commodities Fund,**
**Utalii House - 11th Floor,**
**Utalii Lane, Off Uhuru Highway,**
**S.L.P 52714 – 00200, Nairobi.**

au kupitia baruapepe: info@comfund.co.ke

Maombi yanapasa kupokelewa kufikia **Jumanne, Septemba 5, 2023.** Onyesha nafasi unayowania kwenye bahasha au kichwa cha baruapepe yako.

***Kumbuka: Commodities Fund ni Mwajiri anayezingatia Usawa kwa Wote. Walemavu wanahimizwa kutuma maombi. Ni wale tu watakaoteuliwa tutawasiliana nao. Aina yoyote ya kujipendekeza itafanya ombi lako litupwe nje..***

---

REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF YOUTH AFFAIRS, THE ARTS AND SPORTS

### *STATE DEPARTMENT FOR SPORTS*

### USAJILI WA WAUZAJI NA WATOAJI HUDUMA 2023-2026

Katibu, Idara ya Masuala ya Vijana na Sanaa anaalika maombi ya tenda kwa huduma zifuatazo: -

| S/NO. | NAMBARI YA MAREJELEO | MAELEZO YA HUDUMA NA BIDHAA | WASHIRIKI |
|---|---|---|---|
| | | **MCHUJO WA WAUZAJI** | |
| 1. | MOYAS/SD/PRQ/001/2023-2026 | Kununua na kupeleka Viti vya Ofisi | Wazi |
| 2. | MOYAS/SD/PRQ/002/2023-2026 | Kununua na kusambaza vifaa vya ICT (Kompyuta, Mitambo ya Kuchapisha na vifaa sawa na hivyo) | Wazi |
| 3. | MOYAS/SD/PRQ/003/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Hoteli (Malazi, Vifaa vya Makongamano, Kuandaa upishi wa nje) | Wazi |
| 4. | MOYAS/SD/PRQ/004/2023-2026 | Utoaji wa huduma za ukarabati, utunzaji na urekebishaji wa mitambo ya ICT | Wazi |
| 5. | MOYAS/SD/PRQ/005/2023-2026 | Utoaji wa huduma za ukarabati na utunzaji wa viti na meza za ofisi | Imehifadhiwa |
| 6. | MOYAS/SD/PRQ/006/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Kupiga Chapa na Kutengeneza T-Shati na Kofia | Imehifadhiwa |
| 7. | MOYAS/SD/PRQ/007/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Kukarabati magari na kuyatunza | Imehifadhiwa |
| 8. | MOYAS/SD/PRQ/008/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Uvumishaji bidhaa | Wazi |
| 9. | MOYAS/SD/PRQ/009/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Kuongoza Sherehe | Wazi |
| 10. | MOYAS/SD/PRQ/010/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Mawasiliano | Wazi |
| 11. | MOYAS/SD/PRQ/011/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Uandalizi wa Vipindi | Wazi |
| 12. | MOYAS/SD/PRQ/012/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Kuua wadudu wasumbufu | Wazi |
| 13. | MOYAS/SD/PRQ/013/2023-2026 | Utoaji wa kadi za kupigia simu (Safaricom, Airtel & Telkom) | Imehifadhiwa |
| 14. | MOYAS/SD/PRQ/014/2023-2026 | Utoaji wa Vifaa vya Mawasiliano (Kamera, tripodi etc.) | Imehifadhiwa |
| 15. | MOYAS/SD/PRQ/015/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Usafi | Wazi |
| 16. | MOYAS/SD/PRQ/016/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Bima ya Sherehe | Wazi |
| 17. | MOYAS/SD/PRQ/017/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Usalamas | Wazi |
| | | **MIKATABA YA USHIRIKIANO** | |
| 1. | MOYAS/SD/FC/001/2023-2026 | Ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kuandika | Imehifadhiwa |
| 2. | MOYAS/SD/FC/002/2023-2026 | Ununuzi na usambazaji wa Vifaa vya Michezo | Wazi |
| 3. | MOYAS/SD/FC/003/2023-2026 | Ununuzi na Usambazaji wa Sare za Michezo | Imehifadhiwa |
| 4. | MOYAS/SD/FC/004/2023-2026 | Ununuzi na Usambazaji wa magurudumu na betri za gari | Wazi |
| 5. | MOYAS/SD/FC/005/2023-2026 | Ununuzi wa Maji ya Kunywa | Wazi |
| 6. | MOYAS/SD/FC/006/2023-2026 | Utoaji wa Huduma za Kukodisha Magari | Wazi |
| 7. | MOYAS/SD/FC/007/2023-2026 | Ununuzi na Usambazaji wa Sare | Wazi |

Stakabadhi za Kuchuja/Kusajili Wauzaji na Wanakandarasi zinazoelezea masharti ya utendakazi zinaweza kupatikana katika GRATIS kutoka kwa wavuti ufuatao: **www.ppra.go.ke, www.ppip.go.ke.**

Stakabadhi zilizojazwa na kuwekwa ndani ya bahasha iliyoandikwa nambari za aina ya tenda na maelezo zinapasa kuwekwa ndani ya sanduku la tenda lililoko katika **Supply Chain Management Office, UCHUMI HOUSE 11th Floor** na kutumwa kwa:

**The Principal Secretary,**
**State Department for Sports,**
**P. O. Box 49849-00100,Nairobi.**

mnamo au kabla ya **Agosti 31, 2023 saa 4.00 asubuhi** Maombi/tenda zitafunguliwa papo hapo. Tafadhali kumbuka kwamba, wauzaji wataruhusiwa kuwasilisha ombi moja kwa kila kitengo. Maombi kadha yatapuuzwa.
Hatua yoyote ya kujipigia debe kwa njia yoyote itafanya ombi lako lisishughulikiwe.

**KATIBU**
**IDARA YA MICHEZO**

KENYA VISION 2030

Kenya National Highways Authority

Quality Highways, Better Connections

# CALL FOR APPLICATIONS FOR TVET SCHOLARSHIPS UNDER:

## 1. MULTINATIONAL BAGAMOYO – HOROHORO/LUNGA LUNGA – MALINDI ROAD PROJECT

- PHASE 1: MOMBASA – MTWAPA – KILIFI SECTION

## 2. MOMBASA – MARIAKANI HIGHWAY PROJECT

- LOT 1: MOMBASA – KWA JOMVU SECTION

### 1. BACKGROUND

The Kenya National Highways Authority (KeNHA) is implementing the Multinational Bagamoyo – Horohoro/Lunga Lunga – Malindi Project, Phase 1: Mombasa – Mtwapa – Kilifi (A7) section financed by the African Development Bank (AfDB) and a grant from the European Union (EU). In addition, KeNHA is implementing Lot 1: Mombasa – Kwa Jomvu under financing from the African Development Bank.

Provision of technical and vocational education and training of unemployed youth is a common component in the above-mentioned road projects. The training aims at equipping vulnerable youth within the project areas with skills for gainful work and social sustainability. The training targets youth from the counties of Kwale, Mombasa and Kilifi where the projects traverse.

### 2. ELIGIBILITY CRITERIA

Applications may be submitted by those who meet the following criteria:-

***i. Basic Criteria for Selection for Vocational Skills Training***

a) Must be aged between 18 and 35 years old with no formal training at Diploma level or above;
b) Persons who are able to read and write with KCSE or KCPE Certificates;
c) Persons who may have dropped out of school with no formal training;
d) Consideration of the applicants from low income families and those living in informal settlements within the counties traversed by the project road;
e) Should be a resident of Kilifi, Mombasa or Kwale County.

***ii. Preference will be given to:***

a) Youth who are orphaned and/or those from single parenthood families,
b) Young single mothers who meet the qualifications;
c) Applicants who are categorized as persons living with disability

### 3. SCOPE OF THE SCHOLARSHIP

The scholarship will cover the following: -

i. Tuition and Examination Fee
ii. Material Requirements for the courses
iii. Monthly subsistence allowance for each beneficiary

### 4. COURSES TO BE OFFERED UNDER THE SCHOLARSHIP.

| Institution | Course | Duration | Qualification |
|---|---|---|---|
| **Christian Industrial Training Center (CITC) - Mombasa** | Welding and Fabrication | 3 Months | KCPE and above |
| | Motor Vehicle Mechanic | 3 Months | KCPE and above |
| | Masonry | 3 Months | KCPE and above |
| | Cake, Bread Making & Decoration | 3 Months | KCPE and above |
| | Basic Electrical | 3 Months | KCPE and above |
| | Basic Tailoring | 3 Months | KCPE and above |
| | Computer Operator | 3 Months | KCPE and above |
| | Basic Hair Dressing | 3 Months | KCPE and above |
| **Kenya Coast National Polytechnic (KCNP) - Mombasa** | Electrical Installation (Wireman) | 6 Months | Open |
| | Plumbing & Pipe Fitting | 6 Months | Open |
| | Masonry | 6 Months | Open |
| | Carpentry and Joinery | 6 Months | Open |
| | Hair Dressing Grade III, II or I | 6 Months | Open |
| | Beauty Therapy Grade III, II or I | 6 Months | Open |
| | Motor Vehicle Mechanics Grade III, II or I | 6 Months | Open |
| | Welding & Fabrication Grade III, II or I | 6 months | Open |
| **Mtongwe Vocational Training Centre - Kwale** | Plumber Pipe Fitter | 6 Months | Open |
| | Motor Vehicle Mechanic | 6 Months | Open |
| | Electrical Wireman \ | 6 Months | Open |
| | Computer Operator/ Keyboarding | 3 Months | Open |
| **Mdzongoloni Vocational Training Centre - Kilifi** | Carpentry and Joinery | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Hair Dressing & Beauty Therapy | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Electrical Installation | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Plumbing & Pipe Fitting | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Masonry | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Metal Processing Technology | 12 Months | KCPE/KCSE |
| **Mkwajuni Vocational Training Centre - Kilifi** | Hair Dressing & Beauty Therapy | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Tailoring & Dressmaking | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Computer Applications | 3 Months | KCPE/KCSE |
| | Motor Vehicle Mechanics | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Electrical Installation | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Masonry | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Welding & Fabrication | 12 Months | KCPE/KCSE |
| | Plumbing/ Pipe Fitter | 12 Months | KCPE/KCSE |

### 5. APPLICATION FORMS

Application forms can be downloaded from the KeNHA Website ***(www.kenha.co.ke)*** or hard copies obtained from the KeNHA Coast Regional Offices, Public Works Building, 2nd floor, Mahindi Road off Shimanzi Road, Mombasa County Commissioner's Office, Kilifi County Commissioner's Office and Kwale County Commissioner's Office.

### 6. SUBMISSION OF APPLICATIONS

Application forms by the interested youth MUST be stamped by the Area Chief or Assistant County Commissioner as a verification of the residency status of the applicant.

The duly filled applications should be dropped at any of the following locations: -

- KeNHA Coast Regional Offices, Public Works Building, 2nd floor, Mahindi Road off Shimanzi Road – Mombasa
- Mombasa County Commissioner's Office
- Kilifi County Commissioner's Office
- Kwale County Commissioner's Office

Applications must be submitted by ***Friday 1st September, 2023*** at ***5:00pm.*** Applications received after this deadline will not be considered.

### 7. SELECTION PROCEDURES AND AWARDING OF SCHOLARSHIPS

The selection of applicants will be undertaken with the support of the National Government and County Education Officers in the respective counties. All received application letters will be evaluated against the eligibility criteria. The output of this process will be a list of applicants to be invited for a physical vetting exercise. A list of successful applicants will be generated upon completion of vetting. The applicants will be contacted and enrolled to their respective institutions in the **September 2023 intake.**

Scholarships shall be awarded on the basis of a comparative evaluation of the applications submitted, of the requirements met, and of the criteria relating to the merit established according to a specific evaluation chart.

All inquiries should be addressed to:

Director General
Kenya National Highways Authority
P.O. BOX 49712 - 00100
**NAIROBI**

Attn: **Eng. Cleophas Makau**

**Customer Care Hotline: 020 - 4954000**

**For all your queries email us on:** communication@kenha.co.ke, **Report corruption and unethical conduct:** integrity@kenha.co.ke

**@KeNHAKenya** **Website: www.kenha.co.ke** **Kenya National Highways Authority**

ISO 9001:2015 Certified

# Serikali kutoa ufadhili zaidi kukuza vipaji vya michezo kwa vijana mashinani

NA ROBERT OJWANG(KNA)

Serikali imeahidi kutoa ufadhili zaidi kwa shughuli za michezo ili kusaidia maendeleo ya vipaji mashinani na kuwawezesha wanafunzi kuendeleza vipaji vyao vya michezo.

Katibu wa Elimu ya Msingi, Belio Kipsang, alisema Wizara ya Elimu inalenga kukuza utambuzi wa vipaji na kuendeleza vipaji vya vijana kutoka ngazi ya chini hadi kimataifa. Dkt Kipsang aliwahakikishia wanafunzi kwamba, kupitia Mpango wa Uchumi wa Chini-Kwenda-Juu na Mpango wa Talanta Hela, serikali inalenga kusaidia wanamichezo kufikia utambuzi wa kitaifa na kimataifa na kupata maisha bora kutokana na vipaji vyao.

Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na mkurugenzi katika Wizara hiyo, Hassan Duale, wakati wa sherehe ya ufunguzi wa mashindano ya kitaifa ya shule za msingi katika Shule ya Upili ya Wavulana ya Kisumu, Katibu alitambua jukumu muhimu ambalo michezo na sanaa inatekeleza katika nyanja ya kimataifa.

Mtaala wa Utendaji na Umilisi (CBC), alisema, unachochea maendeleo ya vipaji kwa kuwawezesha wanafunzi wadogo kutambua elimu kamili na kupata ustadi, maadili na maarifa ambayo ni muhimu kuwa mwanamichezo nyota, anayekidhi viwango vya kimataifa.

"Kama Wizara, tunashughulikia kikamilifu jukumu la kutambua na kukuza vipaji miongoni mwa wanafunzi katika ngazi zote ili kuwaweka katika nafasi ya kimataifa na kupata mapato mazuri kutokana na vipaji vyao," alisema Dkt. Kipsang.

> Shule 2,000 zilizoteuliwa zitatumika kukuza vipawa katika maeneo ya mashinani

Aliwapongeza wadau, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Michezo, Sanaa na Maendeleo ya Jamii kwa kusaidia shughuli za Michezo za Mzunguko wa Pili wa kitaifa zinazofanyika katika Kaunti za Kisumu na Kakamega.

Mashindano hayo yamevutia ushiriki wa wanafunzi 756, ikiwa ni pamoja na wasichana 421 na wavulana 335 katika mashindano ya kitaifa ya michezo ya shule za msingi Kisumu.

Mashindano ya kitaifa ya shule za sekondari yanayofanyika Kakamega, yamevuta wanafunzi 1,264, ikiwa ni pamoja na wasichana 592 na wavulana 672 wanaoshindana katika nyanja mbalimbali. Dkt Kipsang alipokea kwa furaha ushirikiano kati ya Shirikisho la Soka Kenya (FKF) na FIFA kuzindua Programu ya Soka kwa Shule ambapo shule za msingi zaidi ya 2,000 nchini kote zinatarajiwa kupokea mipira na vifaa vya mafunzo.



Katibu wa Elimu Msingi, Dkt Belio Kipsang, wakati wa ufunguzi rasmi wa mashindano ya michezo baina ya shule za sekondari katika Kakamega High School. Picha: HISANI

Kupitia programu hiyo, aliongeza, makocha 50 wa shule za msingi waliochaguliwa kutoka kote nchini wanapata mafunzo ili waweze kuwa na ujuzi waa kutosha wa mpira wa miguu na kuwa wakufunzi wakuu katika maeneo yao. "Shule za majaribio 2,000 zilizochaguliwa zitatumiwa kuboresha ustadi wa mpira wa miguu katika ngazi ya chini ili kulingana na viwango vya kimataifa.

Hii inalingana na mtazamo wetu wa chini-kwenda-juu wa ustawi.

Kenya inakusudia kuwa kitovu cha soka wakati mipango hii inashika kasi," alisema.

Dkt Kipsang aliomba pia wadau wengine wenye mtazamo kama huo na uwezo kuungana na serikali katika jitihada zake za kuendeleza vipaji hadi ngazi ya kimataifa.

REPUBLIC OF KENYA

## FINANCIAL REPORTING CENTRE

**OLD MUTUAL TOWER**
**PRIVATE BAG 00200, NAIROBI TEL: +254 709858000**

## Public Survey on Virtual Assets (VAs) and Virtual Assets Service Providers (VASPs)

The Financial Reporting Centre is established under Section 21 of the Proceeds of Crime and Anti-Money Laundering Act (POCAMLA), 2009 with the principal objective being to assist in the identification of the proceeds of crime and the combating of money laundering and terrorism financing.

The Financial Reporting Centre together with other government institutions and private sector players, invites the public to take an anonymous survey on Virtual Assets and Virtual Asset Service Providers operations in Kenya. Virtual assets and associated activities have grown rapidly around the world over the recent years. While this space has the positive potential to spur financial innovations and efficiency, it can also present opportunities for illicit activities like money laundering and terrorism financing among others.

As part of the mission to protect the integrity of our financial system and contribute to the safety of our citizens, the Financial Reporting Centre is inviting the public to share their thoughts through a short survey, to help understand the Kenyan ecosystem of virtual assets activities and service providers, along with their benefits and the potential money laundering & terrorism financing risks.

Your feedback will play a vital role in shaping the future of the virtual assets ecosystem and promoting a safer and more transparent financial system. The FRC appreciates your participation and looks forward to receiving your input by **8th September 2023.** Please go to FRC's Website: **www.frc.go.ke** to participate.

For more information, kindly send an email to, **nrakenya@frc.go.ke**

**DIRECTOR GENERAL**
**FINANCIAL REPORTING CENTRE**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA
KNBS KENYA NATIONAL BUREAU OF STATISTICS *Keeping you informed*

## KENYA NATIONAL BUREAU OF STATISTICS

## VACANCY ANNOUNCEMENT

The Kenya National Bureau of Statistics (KNBS) is a State Corporation established via the Statistics Act No. 4 of 2006. KNBS is the principal government agency for collecting, analyzing and disseminating statistical data and is the custodian of official statistical information in Kenya.

The Bureau wishes to recruit a dynamic, result oriented and self-driven individual to fill the vacant position as outlined below.

| POSITION | VACANCY NO. | GRADE | NO. OF POSITIONS |
|---|---|---|---|
| DIRECTOR, CORPORATE SERVICES | KNBS/DCS/4/2023 | Level 2 | 1 |

Applicants should fill and submit a copy of the employment application form **Ref. KNBS/F/93/29** availabe on the KNBS website **www.knbs.or.ke** Full details of the job description and specifications are contained on the website **www.knbs.or.ke** The form should be accompanied by copies of academic, professional and other relevant certificates, transcripts and testimonials.

The reference number for the post should be clearly marked on the envelope and addressed to:

**The Director General**
**Kenya National Bureau of Statistics**
**P. O. Box 30266 – 00100**
**Real Towers, Upper Hill, 4th floor**
**Hospital Road**
**NAIROBI**

Applications must be received not later than **5th September, 2023**. Only candidates who have met all the requirements of the advert and have been shortlisted will be contacted.

**Kenya National Bureau of Statistics is an Equal Opportunity Employer. Canvassing will lead to automatic disqualification.**

***Women, Persons With Disabilities, the marginalised and minorities are encouraged to apply.***

KENYA VISION 2030

# Njaa magugu ya striga yakiharibu mashamba ya mahindi na mtama

NA ABSALOM NAMWALO(KNA)



**Shamba la Christopher Emukule, mkulima wa mtama katika eneo la Moding ambaye shamba lake liliathiriwa na magugu aina ya Striga maarufu kama "Luyongo".**

Wakulima katika kaunti ya Busia wameoa wito kwa serikali kuingilia kati na kusaka suluhisho kwao baada ya mashamba yao ya mahindi na mtama kuvamiwa na magugu hatari ya striga ambayo yanatishia usalama wa chakula katika eneo hilo.

Ziara ya KNA kwenye mashamba yaliyoathiriwa haswa eneo la Teso Kaskazini na Teso Kusini, Amagoro, imebaini kuwa, magugu hayo yamesambaa katika mashamba yaliyopandwa haswa na mahindi na mtama. Magugu haya yameacha wakulima wengi kuomba serikali za kaunti na kitaifa kushirikisha taasisi za utafiti na wanasayansi kupata suluhisho la kudumu kwa tatizo hilo.

Kwa kudumisha mimea, magugu haya yamesababisha mashamba mengi kuonekana kuwa na maua huku mahindi na mtama yakiathirika, hivyo kufanya iwe vigumu kwa mimea kukomaa na kuzalisha mazao. Mvua ya majira mafupi tayari imepita.

Christopher Emukule, mkulima wa mahindi na mtama eneo la Moding ni mkulima mwenye huzuni anapoelezea jinsi magugu hayo yamefanya mahindi kwenye shamba lake kuwa madogo na mengine kukaukha kuanzia juu. Inayojulikana kwa jina la "Luyongo" katika Kikhayo, lugha ya kabila la Luhya, magugu hatari yanaenea haraka na ikiwa uzalishaji wake hautadhibitiwa, yanaweza kuenea kwenye shamba katika msimu wa kupanda ndani ya misimu mitatu tu.

"Ni jambo la kusikitisha kuwa, mashamba mengi hapa yanapata madhara makubwa kutoka kwa magugu haya. Mimea inaonekana midogo na maua mengi yenye mvuto kutoka kwa magugu inayoonekana kutoka mbali, ithibati ya kutokuwa na matumaini kwa wakulima," alisema Emukule.

Magugu ya striga, ambayo yanapata maji na virutubisho kutoka kwa mimea kwa ajili ya ukuaji wake, husababisha ukuaji mdogo wa mahindi kwa kushikamana na mizizi yake kwenye mmea mwenyeji na kufyonza virutubisho muhimu na unyevu kwa ukuaji wake.

Yanenea kwa kutoa mbegu ambazo huchipuka katika msimu wa kupanda ufuatao, hivyo kuwa vigumu kudhibiti. Harakati za wanyama kwenye shamba pia husaidia kuenea kwake.

Vitalis Etyang, mkulima huko Amagoro, amewahimiza wakulima wengine wa mahindi katika kaunti kutumia kilimo cha mseto na mchanganyiko ambacho ni njia ya jadi ya kupunguza magugu shambani. Maharagwe ni mazao bora kwa kilimo cha mseto kwani husaidia kuingiza naitrojeni na kupunguza nafasi ya kuwepo kwa magugu ya striga shambani.

Gavana wa Busia, Paul Otuoma, alisema ana mpango wa kuhakikisha kila nyumba ina ghala la kuhifadhia nafaka kwani kaunti ina uwezo wa kutatua umaskini kwa kuzalisha chakula cha kutosha. "Tunakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula cha kuwalisha watu wetu," Otuoma alisema.

# Serikali yazindua ripoti ya athari kuhusu mradi wa mtandao shuleni

NA HAMDI MOHAMUD(KNA)



**Dkt. Belio Kipsang atuza mmoja wa washindi wa kwanza katika kitengo cha video kutoka Friends' School Kamusinga. Picha: Hamdi Mohamud**

Wizara ya Elimu kwa Ushirikiano na UNESCO na Huawei imezindua ripoti ya tathmini kuhusu athari za mradi wa majaribio wa uunganisho wa mtandao kwa shule zilizochaguliwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT Authority) mnamo 2021.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ripoti hiyo katika Shule ya Friends Kamusinga, Katibu wa Elimu ya Msingi Dkt. Belio Kipsang alisema, "huku serikali ikijitahidi kupanua usambazaji wa mtandao kwa shule zote nchini kulingana na Mpango Mkuu wa Dijitali na Nguzo ya Barabara Kuu ya Dijitali ya Ajenda ya Kubadilisha Uchumi Chini kwenda Juu (BeTA), ripoti hii itaongoza jitihada hizo ili kuhakikisha athari za kujifunza na walimu zinakuwa kubwa kwa wanafunzi na walimu kote nchini."

Aliendelea: "Ripoti imegundua wazi kuwa, mtandao unaboresha upatikanaji wa elimu sawa kwa wanafunzi katika maeneo ya vijijini, haswa wasichana na wale wenye ulemavu. Napenda kushukuru Huawei kupitia mradi wao wa TECH4ALL na UNESCO kwa ushirikiano wao na serikali katika kutoa uunganisho endelevu wa mtandao wa WI-FI, na kwa kusaidia ripoti hii muhimu ya tathmini," aliongeza. Kulingana na ripoti, asilimia 98 ya wanafunzi walionyesha kuwa mtandao unakidhi mahitaji yao, huku shule zikiripoti kuwa zimeokoa Shilingi 120,000 kwa vifurushi vya data za simu.

Zaidi ya hayo, asilimia 84 ya wanafunzi walisema mtandao unafanya kujifunza kufurahisha zaidi, asilimia 71 walisema inafanya mawazo magumu kuwa rahisi kuelewa, asilimia 54 walisema inafanya masomo kuwa ya kuvutia, asilimia 23 walisema intaneti inafanya kujifunza kuwa wa kufurahisha, na asilimia 13 walisema inaongeza idadi ya wanaohudhuria mafunzo darasani.

> "Intaneti inaweza wanafunzi kupata elimu ya hali ya juu" Ripoto

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Bw. Joshua Opondo alisema, "serikali tayari imekamilisha mpango wa kina wa kupanua uunganisho wa mtandao, na shule zinalengwa kunufaika zaidi kwenye programu hiyo.

Tumeunganisha hospitali kadhaa, vyuo vikuu, na Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi kwenye mtandao wetu wa NOFBI," alisema.

REPUBLIC OF KENYA

nema
mazingira yetu | uhai wetu | wajibu wetu

## PUBLIC NOTICE

**IN THE MATTER OF THE STATUTORY INSTRUMENTS ACT (NO. 23 OF 2013)**
**AND**
**THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT AND CO-ORDINATION ACT (NO. 8 OF 1999)**

**NOTIFICATION OF REGULATORY IMPACT STATEMENTS ON PROPOSED ENVIRONMENTAL MANAGEMENT REGULATIONS, 2023**

Pursuant to Section 8 of the Statutory Instruments Act (No. 23 of 2013), the Director General National Environment Management Authority (NEMA) hereby notifies the general public that Regulatory Impact Statements on the underlisted proposed Environmental Management Regulations have been prepared to assess the impact of the Regulations on the community and businesses.

a) Environmental Management and Coordination (Waste Management) Regulations;
b) Environmental Management and Coordination (Water Quality) Regulations;
c) Environmental Management and Coordination (Noise and Excessive Vibrations (Control) Regulations;
d) Environmental Management and Coordination (Biodiversity, Access to Genetic Resources and Benefit Sharing) Regulations;

**The general objective of the proposed Regulations is to:**

- To align the regulations with the provisions of the Constitution of Kenya;
- Reduce environmental damage and facilitate economic development and socio- economic benefits;
- Create an enabling environment for employment in the green economy and to promote circularity in environmental management;
- Establish an environmentally sound infrastructure and systems for sustainable waste management; and
- Improve the health of all Kenyans by ensuring a clean and healthy environment.
- To update the existing regulations and capture emerging threats and opportunities.

This is therefore to require all persons likely to be affected by the proposed Regulations to submit written comments so as to reach the undersigned not later than fourteen **(14) days** from the date of publication of this notice.

The draft Regulatory Impact Statements and the draft proposed Regulations are available under NEMA's website h**ttps://www.nema.go.ke/** and also available upon request through the email: **emcareview@gmail.com** during normal working hours.

The public is also invited to make comments on the Regulations and Regulatory Impact Statement by way of snail mail or email by submission of a written memorandum to the email address at: **emcareview@gmail.com.**

The Authority welcomes any stakeholder who would prefer virtual interaction on the subject matter to notify us through the email address given in order for the Authority to prepare for such meetings. The Authority shall schedule virtual and/or physical meetings as circumstances may allow on dates and venues to be communicated to members of the public to discuss the comments received.

Please send your written comments to:

**The Director General**
**National Environment Management Authority, (NEMA HQ)**
**Popo Road, South C, off Mombasa Road**
**P.O.BOX: 67839-00200,**
**NAIROBI**

**OR**
**Email: emcareview@gmail.com**
**Contact: +254 20 2183718/62101370**

**Report Environmental Complaints through; Tel: 0741 101 100 / 0786 101 100, Email: incidence@nema.go.ke**

ISO 9001 BUREAU VERITAS Certification

@NemaKenya

KENYA VISION 2030

MyGov.
AGOSTI 15, 2023
NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 7/2023-2024

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

# Serikali kuinua uzalishaji wa kahawa ikilenga soko la kimataifa

**NA WANGARI NDIRANGU(KNA)**

Serikali imeanzisha mipango mipya ya kuchochea uzalishaji wa kahawa ndani ya miaka mitano ijayo ili kupanua mapato yake katika soko la kimataifa la kahawa.

Ili kufanikisha hayo, Katibu wa Vyama vya Ushirika, Patrick Kilemi, alifichua kuwa , Serikali imejitolea kuhamasisha uzalishaji wa kahawa kutoka tani 51,000 za sasa hadi tani 81,000 ifikapo 2024 na hatimaye hadi tani 260,000 ifikapo 2027.

"Tutafanikisha hili kwa kupunguza gharama za uzalishaji kupitia ruzuku kwa pembejeo za kilimo, kusawazisha upatikanaji na ugawaji wa Mfuko wa Mapema wa Mazao ya Kahawa katika New KPCU na kuimarisha utafiti wa kahawa kupitia kuanzishwa upya kwa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa," Kilemi alisema.

Katibu alitoa maoni hayo wakati wa warsha ya kujifamahamisha na opereshеni za Mfumo wa Uthibiti wa Moja kwa Moja (DSS), jukwaa la teknolojia ambalo biashara ya kahawa itafanywa hivi karibuni kama ilivyoainishwa katika utaratibu mpya wa biashara ya kahawa unaosimamiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mtaji (CMA).

Aliongeza kuwa serikali itaendeleza upya uanzishwaji wa Bodi ya Kahawa ya Kenya ili kuangalia na kuratibu sera ya kahawa, hasa kuweka kahawa ya Kenya kimataifa na kufanya kazi na serikali za kaunti kuimarisha huduma za upanuzi.

"Tungependa kuwaalika wafanyabiashara na wanunuzi wa kahawa, wa ndani na kimataifa, kuunga mkono wakulima na serikali kwa kutoa bei inayolingana na juhudi za wakulima shambani na ubora wa kahawa yetu," aliongeza.



Katibu Patrick Kilemi



> “Takwimu hizi zinaonyesha kibarua kinachotusubiri katika sekta ya kahawa -Kilemi

Kilemi alikumbuka kwamba, kati ya 1984 na 1990, sekta ndogo ya kahawa iliunda karibu asilimia 30 ya fursa za ajira katika sekta ya kilimo.

Ardhi chini ya kilimo cha kahawa nchini Kenya mnamo 1963 ilikuwa ekari 45,000 na uzalishaji wa tani 43,778 za kahawa safi. Ekari chini ya kilimo cha kahawa, aliongeza katibu iliongezeka hadi ekari 170,000 mnamo 1987/1988 na uzalishaji wa juu kabisa wa tani 129,637 za kahawa safi lakini ulipungua hadi takriban ekari 116,000 na uzalishaji wa jumla wa tani 36,867 mnamo mwaka 2019/2020.

"Hizi takwimu zinaonyesha wazi kazi tunayopaswa kufanya kama sekta," alisema. Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Kahawa la Nairobi (NCE), Lisper Ndungu, alitangaza uteuzi wa Benki ya Ushirika ya Kenya kama mtoa huduma wa DSS ili kurahisisha malipo ya mapato kwa wakulima wa kahawa nchini.

Watumiaji wa soko la kahawa -wakala wa kahawa, wafanyabiashara, wamiliki wa maghala, wakulima wa kahawa na watoa huduma wengine, walifunzwa na Sekretarieti ya NCE na idara ya kahawa kuhusu utendaji wa DSS.

Waziri wa Fedha na Mipango wakati huo Ukur Yatani mnamo Aprili 3, 2020 alitangaza Kanuni za Masoko ya Mitaji (Kahawa), Kanuni za 2020, ambazo ziliweka NCE na wanachama wake chini ya usimamizi wa udhibiti wa CMA.

## KWA UFUPI

### Kaunti ya Homa Bay, yazindua mpango wa maendeleo wa miaka 5

Kaunti ya Homa Bay, imezindua mfumo wa maendeleo wa miaka mitano unaolenga kuchochea uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi.

Gavana Gladys Wanga alizindua Mpango wa Maendeleo wa Pamoja wa Kaunti (CIDP) wakati wa hafla iliyofanyika mjini Homa Bay. Mipango hiyo inaelezea miradi ya maendeleo iliyojumuisha ya serikali ya kaunti kwa kipindi cha 2023-2027.

Bi Wanga alionyesha maeneo kadhaa ya kuzingatia ndani ya CIDP, ikiwa ni pamoja na kufufua mazao yaliyotelekezwa kama mtama, mawele, na muhogo. “Utawala wangu unakusudia kutunga na kufuatilia sheria na sera za kilimo ili kuboresha uzalishaji wa mazao na mifugo,” alisema.

Katika sekta ya afya, kaunti inalenga kutokomeza magonjwa ya kuambukiza, kushughulikia mzigo wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, kutoa huduma za matibabu muhimu, na kupunguza hatari za afya kwa wakazi.

CIDP pia ina mipango ya makazi na maendeleo ya miji ili kutoa malazi ya gharama nafuu na yanayofaa kwa wakazi. Biashara na utalii vinakusudiwa kukuza kupitia uboreshaji wa vivutio vya watalii na kuunda mazingira mazuri ya biashara na lengo la kuunda utajiri, kupunguza umaskini, na kuunda ajira.

Gavana Wanga alitaja ndoto za kaunti kuhusu ujenzi wa barabara na lengo la kuinua mji wa Homa Bay kuwa jiji ifikapo 2034. Hafla ya uzinduzi ilihudhuriwa na Naibu Gavana Oyugi Magwanga, Seneta Moses Kajwang, na Mwakilishi wa Wanawake Joyce Osogo.

Gavana Wanga alisisitiza kwamba, CIDP ni mwongozo wa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa miaka mitano ijayo na ilibuniwa kwa mchango wa wakazi wa kaunti kupitia mchakato kamili wa ushiriki wa umma, kuanzia ngazi ya kijiji.

Mpango wa maendeleo unalenga kufanya Kaunti ya Homa Bay kuwa tajiri na unazingatia mbinu inayoongozwa na wananchi. Ushirikiano kati ya wakazi na maafisa wa kaunti ni muhimu kwa utoaji wa huduma wenye mafanikio na kufikia malengo yaliyotambuliwa ya maendeleo. Uongozi wa kaunti pia ulisisitiza umuhimu wa kupambana na ufisadi ili kuhakikisha utekelezaji wa ufanisi wa CIDP.

*Na Davis Langat (KNA)*

### Serikali kuanzisha Kituo cha Uokoaji wa Baharini

Serikali itaanzisha Kituo cha Uratibu wa Uokoaji wa Baharini (MRCC) jijini Kisumu ili kushughulikia usalama wa watumiaji wa Ziwa Victoria.

Akitangaza hayo, Katibu wa Usafirishaji na Maswala ya Baharini Bw. Shadrack Mwadime, alisema Sh. 350M zimetengwa kwa ujenzi wa Kituo hicho katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

Bw. Mwadime alifichua hayo alipoongoza kikao cha Kamati ya Mwongozo ya Mawasiliano na Usafirishaji wa Baharini wa Ziwa Victoria Kenya katika ofisi yake, ambapo mwenzake wa Idara ya Masuala ya Afrika Mashariki, Bw. Dubat Abdi pia alihudhuria.

Aidha, Mwadime alisema Serikali itajenga Vituo vinne vya Utafutaji na Uokoaji (SARS) katika Kaunti zinazopakana na ziwa za Migori, Homabay, Siaya na Busia, ambavyo vitasheheni boti za uokoaji wa haraka na wafanyakazi waliofundishwa kutoa huduma ya kwanza katika visa vya ajali kwenye Ziwa.

"Kituo cha Uratibu na Vituo vya Utafutaji na Uokoaji vitashughulikia usalama na usafirishaji wa baharini kupitia utoaji wa mfumo wa usafirishaji na mawasiliano salama, ufanisi, nafuu na utunzaji wa mazingira ndani ya nchi za Afrika Mashariki zinazoshiriki Ziwa", alisema Katibu wakati wa kikao ambapo kamati pia ilidhinisha mradi huo.

Mradi wa Mawasiliano na Usafirishaji wa Baharini wa Ziwa Victoria nchini Kenya ni mrithi wa Mradi wa Mawasiliano na Usafirishaji wa Baharini wa Ziwa Victoria wa kimataifa ambao ulianzishwa mnamo 2010 na ulikuwa unategemewa kutekelezwa kwa mpango kikanda na nchi za Afrika Mashariki zinazoshiriki Ziwa Victoria.

Hata hivyo, mradi huo wa kimataifa uliogharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kima cha Sh. Bilioni 3.6, ulikumbwa na changamoto za kiufundi na muundo ambazo ziliziua utekelezaji wa mradi huo. Hii ilisababisha Kenya kujiondoa katika muundo wa kikanda na badala yake kuutekeleza sehemu yake ya mradi kitaifa.

*Na Julius Ndegwa (PCO)*

# Uzinduzi wa miradi mitano ya ICT kuleta msisimko wa kiuchumi kaunti za Pwani

**NA EVALYNE GITHINJI (PCO)**

Serikali imezindua miradi mitano ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kukuza maendeleo ya kiteknolojia na kustawisha uchumi katika eneo la Pwani.

Miongoni mwa miradi iliyozinduliwa na Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia na Uchumi Dijitali, Eliud Owalo, ni Ofisi ya Kamishna wa Ulinzi wa Takwimu (ODPC) eneo la Mombasa. Owalo pia alizindua Maabara ya Kidijitali ya Jitume katika Coast National Polytechnic na vituo vitatu vya mtandao wa Wi-fi vya umma katika masoko ya Marikiti, Diani na soko jipya la Magongo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa miradi hiyo, Owalo alisisitiza umuhimu wa kuhakikisha usiri na usalama wa Wakenya hauingiliiwi na maendeleo ya kiteknolojia.

"Teknolojia lazima ipatikane kwa urahisi pamoja na faragha na usalama katika chombo kimoja, na tunapokaribisha faida za mapinduzi ya kidijitali, lazima pia tuheshimu haki za watu binafsi na taasisi kuwa na data zao zinazoshughulikiwa kwa uwajibikaji na maadili," alisema.



**Waziri wa Habari, Teknolojia na Uchumi Dijitali Eliud Owalo (pili kushoto) akiongea na wanafunzi wakati wa uzinduzi wa Jitume Digital Lab katika Kenya Coast National Polytechnic. Piha na Beverlyne Musili.**

Waziri alitambua kuwa Ofisi mpya ya Kamishna wa Ulinzi wa Takwimu katika ofisi ya mkoa wa Pwani itatumika kama kitovu cha habari, mwongozo na msaada kwa biashara ndani ya eneo hilo. "Itawawezesha watu binafsi na mashirika kuingiliana kwa ujasiri juu ya usalama wa data yoyote ya kibinafsi ambayo wanaweza kubadilishana katika mchakato huo," alisema. Owalo alihimiza wadau kushirikiana na ODPC kuimarisha imani katika usindikaji wa data ya kibinafsi.

Aidha, alisema mashirika ya serikali, makampuni binafsi, mashirika ya kiraia na raia, wote wana jukumu muhimu katika kujenga mfumo thabiti wa ulinzi wa data nchi nzima.

REPUBLIC OF KENYA
GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
**DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD**
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke